

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

Barua Zote Zitumwe Kwa Mkurugenzi Wa Halmashauri

S.L.P 30112
SIMU Na: 023 - 240 2886
FAX Na: 023 - 240 2007



OFISI YA MKURUGENZI
WA MJI KIBAHA

Kumb. Na. KTC/S. 20/13/83

09/07/2015

Watendaji wa Kata wote
Watendaji wa Mitaa wote
Halmashauri ya Mji
KIBAHA

YAH: KUWASILISHA MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

Rejeeni Somo hapo juu.

Halmashauri ya Mji Kibaha imekamilisha mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao tayari umeidhinishwa na Baraza la Madiwani la tarehe 08/07/2015.

Kwa barua hii tunawasilisha nakala za Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa kila Mtaa na Kata ili uweze kufahamika kwa wananchi wote walipo maeneo yenu.

Watendaji wa Kata na mitaa mnasisitizwa kuhakikisha kuwa wananchi wanafahamishwa kuhusu mkataba huo ili waweze kufahamu haki zao.

Nawatakia utekelezaji mwema

George P. Mbogo
**K. N. Y. MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**

Nakala

Wenyeviti wa Mitaa - kwa taarifa
Halmashauri ya Mji Kibaha,
S. L. P. 30112,
KIBAHA .

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KIBAHA TOWN COUNCIL



MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA
FY 2014/2015

Prepared by:-

Town Director's Office,
P.O.Box 30112,
KIBAHA.

Tel. No. 023 - 240 - 2886
Fax. No. 023 - 240 - 2007

TABLE OF CONTENT

TABLE OF CONTENT	i
DIBAJI.....	iii
CHAPTER ONE	1
1.0 DIRA NA DHAMIRA.....	1
1.5 MAADILI MUHIMU.....	4
CHAPTER TWO	6
2.0 VIWANGO VYA HUDUMA	6
2.1 IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA.....	6
2.2. KITENGO CHA SHERIA.....	8
2.3. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI.....	8
2.4. KITENGO CHA MANUNUZI.....	9
2.5. KITENGO CHA UCHAGUZI	9
2.6. KITENGO CHA NYUKI	9
2.7. KITENGO CHA TEKNOLOGIA, HABARI NA MAWASILIANO	10
2.8. IDARA YA FEDHA NA BIASHARA	11
2.9. IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI.....	15
2.10. IDARA YA ELIMU YA MSINGI	16
2.11. IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI.....	17
2.12. IDARA YA MAENDELEO YA JAMII ,VIJANA NA USTAWI WA JAMII.....	17
2.13. IDARA YA KILIMO NA USHIRIKA.....	21
2.14. IDARA YA ARDHI, MALIASILI NA MIPANGO MIJI.....	22
2.15. IDARA YA MIFUGO NA UVUVI.....	25
2.16. IDARA YA UJENZI.....	26
2.17. IDARA YA MAJI.....	27
2.18. IDARA YA AFYA	28
2.19. IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA	30
CHAPTER THREE	31
3.1. WAJIBU WA HALMASHAURI KWA MTEJA.....	31

3.1 Haki Na Wajibu Wa Mteja	32
3.2 UFUATILIAJI WA MALALAMIKO	33
3.3 JINSI YA KUTUMA MALALAMIKO	33
3.4 KUMBUKUMBU ZA MALALAMIKO.....	33
3.5 NAMNA YA KUTOA MSHINDONYUMA KUHUSU MKATABA HUU	33
3.6 KUKATA RUFAA	34
3.7 MAPITIO YA MKATABA.....	34

DIBAJI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Kibaha imeandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Mkataba wa Huduma kwa Mteja ni kiungo kati ya utendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na wateja wanaopata huduma kutoka katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji katika kutekeleza majukumu yake, Majukumu ya Ofisi hii nikuwezesha wakazi wa Mji wa Kibaha kutekeleza shughuli za Kiuchumi, kijamii na maendeleo katika mazingira bora. Wakazi wa Mji wa Kibaha wanatarajia kupata huduma zenye viwango vya hali ya juu kutoka Serikalini.

Madhumuni ya mkataba huu ni kuufahamisha Umma huduma zitolewazo, viwango vya huduma, taratibu za kuzipata na mahusiano yao na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Aidha, mkataba unaainisha muda wa utoaji wa huduma, mahali zinapotolewa na mtiririko wa kushughulikia masuala mbalimbali yanayojitokeza. Mkataba wa Huduma kwa Mteja unaendana na jitihada za Serikali ya awamu ya Nne za kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuboresha maisha yao.

Mkataba huu utawezesha watumishi na wadau kubadilika kifikra ili kuleta ufanisi, kuimarisha usimamizi, utekelezaji unaojali tija na kuondoa urasimu usio wa lazima. Matarajio ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji ni kutoa huduma iliyo bora kwa kushirikiana na wakazi wa Mji Kibaha ili kujiletea maendeleo.

Kama yalivyoainishwa kwenye Katiba Ya Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania Ibara ya **145** kwamba--- Kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila mkoa, wilaya, mji na kijiji, katika Jamhuri ya Muungano---- na Ibara ya **146**.-inazungumzia madhumuni kama ifuatavyo:-(1) Madhumuni ya kuwapo Serikali ya Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. ----Chombo cha Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia masharti ya sheria iliyokianzisha, kitahusika na shughuli zifuatazo –

- (a) Kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake;
- (b) Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi; na
- (c) Kuimarisha demokrasi katika eneo lake na kuitumia demokrasi kuharakisha maendeleo ya wananchi.

.....
JENIFA OMOLO,
MKURUGENZI WA MJI,
KIBAHA

CHAPTER ONE

1.0 DIRA NA DHAMIRA

1.1 DIRA

Halmashauri ya Mji kibaha kuwa Taasisi ya Umma yenye nguvu na inayoweza kuhimili ushindani wa Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni.

1.2 DHAMIRA

Halmashauri ya Mji Kibaha inachukua jukumu la kufanikisha Uchumi wa Halmashauri ,Kupunguza umaskinin kwa kutoa huduma kwa wanainchi wake kwa wakati kwa kutumia rasilimali zilizopo na michango ya wadau wengine kwa ufanisi na umakini.

1.3 MADHUMUNI YA MKATABA

Lengo kuu la mkataba huu ni kuhusu uwepo na ubora wa huduma zinazotolewa na Halmashauri ya Mji Kibaha. Mkataba huu unafahamisha wadau wetu tuliyojipangia kufanya, jinsi ya kuwasiliana nasi, nini cha kutegemewa kuhusiana na huduma zetu, na jinsi ya kutoa maoni na malalamiko. Mkataba huu utawezesha kushirikisha wadau katika kuongoza Halmashauri. Mkataba pia utaonyesha mwelekeo kwa wateja wetu jinsi ya kudai haki zao katika Halmashauri yetu na pia utaonyesha uwazi katika kuwasiliana, kulalamika na upatikanaji wetu.

1.4 HUDUMA ZITOLEWAZO

Majukumu ya Halmashauri ya Halmashauri ya Mji Kibaha

Halmashauri ya Mji Kibaha inatoa huduma mbalimbali kwa wadau wake kama ifuatavyo;

- Kuajiri na kushughulikia maombi ya uhamisho wa watumishi na kuratibu utoaji wa huduma;
- Kuratibu masuala ya utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa;

- Kukusanya mapato na kudhibiti mapato na matumizi kwa kufanya malipo ya huduma na bidhaa;
- Kulinda, Kudhibiti na kuendeleza Rasilimali za Halmashauri.
- Kuendeleza na kuboresha mipango miji, maendeleo ya ardhi, kilimo na mifugo mjini, maliasili na mazingira;
- Kusimamia ujenzi wa miundombinu ya barabara, majengo, umeme na maji;
- Kuimarisha na kuendeleza shughul za biashara, viwanda, masoko na sekta isiyo rasmi;
- Kuboresha maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na ushirika;
- Kuratibu uibuaji wa miradi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- Kutoa huduma za afya tiba, kinga na kudhibiti taka ngumu na taka maji;
- Kutoa elimu ya msingi na sekondari;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu;
- Kusimamia utekelezaji wa sheria za nchi na sheria ndogo ndogo zilizotungwa na Halmashauri;
- Kuratibu shughuli za burudani, michezo na maendeleo ya vijana;
- Kuratibu mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya ukimwi;

1.4.1 MISINGI YA UTOAJI HUDUMA

Ili kutekeleza mkataba huu, Halmashauri itazingatia mambo yafuatayo katika kutoa huduma kwa wateja;

1.4.2 Kuweka viwango vya huduma

Viwango vya huduma zetu zitawekwa wazi kwa wateja ili waweze kufuatilia na kutathmini utendaji wetu wa kazi.

1.4.3 Kuwa wazi na kutoa taarifa zote

Tutakuwa wazi katika kutoa huduma zetu kwa wateja, kuwasaidia wateja na kuwapatia taarifa zote kuhusu huduma zetu, gharama zetu na mafanikio yetu ya kila mwaka.

1.4.4 Kushirikisha wengine

Tutashirikiana na kushauriana na wateja wetu pamoja na watumishi na kutumia ushauri mzuri utakaotolewa katika kuboresha huduma zetu.

1.4.5 Kuwatendea haki wote

Tutawatendea haki wateja wetu wote, tutaheshimu utu wao, na haki zao binafsi, kuwasaidia kila iwezekanavyo na kutoa kipaumbele kwa wenye mahitaji maalumu.

1.4.6 Kukuza upatikanaji huduma

Tutatoa huduma zetu kwa wateja kwa haraka na kwa urahisi na wateja wetu watapewa fursa ya kuchagua huduma. Tutakuza matumizi ya teknolojia kadiri ya uwezo wetu.

1.4.7 Kutatua matatizo yanaojitokeza

Tutatatua matatizo yatakayojitokeza haraka iwezekanavyo na malalamiko yote yatakayowasilishwa yatashughulikiwa kwa uwazi.

1.4.8 Matumizi bora ya rasilimali

Tutatumia rasilimali kiufanisi na itakayotoa matunda mazuri kwa walipa kodi, wafadhili na wateja wote.

1.4.9 Kuboresha huduma

Tutatafuta kwa bidii njia bora zaidi za kutoa huduma zetu.

1.4.10 Kushirikiana na watoa huduma wengine

Tutafanya kazi na Wizara, Idara na Wakala mbalimbali pamoja na watoa huduma wengine kuhakikisha kuwa huduma zetu ni rahisi kutumika na bora. Halmashauri ya Mji Kibaha inawajibika moja kwa moja kwa masuala ya UKMWI (HIV/AIDS), usawa na jinsia na mifumo ya utawala ya wafanyakazi wa Umma.

1.5 MAADILI MUHIMU

Ili utumishi wa Halmashauri uwe wenye ufanisi na wa kuheshimika, watumishi wanapaswa kuzifuata kanuni za maadili ya utumishi pamoja na kuwa na tabia na mwenendo unaozingatia mambo yafuatayo:

- Kutoa huduma bora.
- Utii kwa serikali.
- Bidii ya kazi.
- Kutoa huduma bila upendeleo.
- Staha kwa wananchi.
- Uaminifu.
- Kuheshimu sheria: na
- Matumizi bora ya taarifa za kazi

1.6 WATEJA WETU

1.6.1 WATEJA WA HALMASHAURI NA MATARAJIO YAO:

MAJINA YA WATEJA/WADAU	MATARAJIO KUTOKA HALMASHAURI
Watumishi wa Halmashauri	<ul style="list-style-type: none">☞ Utawala bora☞ Amani na Utulivu☞ Usalama kazini☞ Mazingira bora na mazuri ya kazi☞ Fursa za kuiendeleza☞ Kupata mshahara na maslahi mengine kwa wakati☞ Kupata mafao ya kustaafu kwa wakati☞ Usawa kwa wote na uongozi mzuri uliotukuka☞ Kuendelezwa kitaaluma☞ Miundo sawa ya kazini inayohamasisha

MAJINA YA WATEJA/WADAU	MATARAJIO KUTOKA HALMASHAURI
	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Mfumo mzuri wa kudhibiti nidhamu kazini ☞ Mwongozo wa wazi na wa kiushindani wa uajiri, uteuzi na upandishaji vyeo ☞ Mfumo ulio wazi wa utathmini wa utendaji kazi Kuwazawadia wanaovuka malengo
OWN – TAMISEMI, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Utoaji wa tafsiri sahihi za sera, sheria na mikakati mbalimbali pamoja na kuratibu LGAs ☞ Ufuatiliaji wa makini wa sera za kitaifa ☞ Uratibu wa utoaji taarifa za huduma zianazotolewa na Halmashauri kwa wizara mbalimbali ☞ Kuwa kiungo kati ya wizara za kisekta na halmashauri
Vyama vya Siasa	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Tafsiri ya sera mbalimbali ☞ Utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ☞ Utawala bora ☞ Utekelezaji wa kazi za serikali ☞ Kushirikishwa; ☞ Takwimu sahihi; ☞ Uwazi; ☞ Haki sawa kwa wote; ☞ Kuzingatia maoni ya wananchi; na ☞ Kufanikisha mipango ya serikali
Madhehebu, Vikundi na Taasisi za Dini, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali, Vyombo vya Habari, Washirika na Wahisani katika Maendeleo	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Ushauri wa kitaalam ☞ Uhusisiano wa karibu wa kuwajali ☞ Kulipwa kwa wakati mara naada ya kutoa huduma ☞ Ufanisi, Uadilifu, nidhamu ya watumishi ☞ Kutoa wataalam ☞ Matumizi mazuri ya fadha ☞ Kuratibu miradi inayopatiwa fedha ☞ Taarifa sahihi na kwa wakati ☞
Wananchi kwa Ujumla wao	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Kushughulikia mahitaji na Majibu ya kero na matatizo kwa wakati ☞ Kufahamu sera na malengo ya serikali ☞ Uwekaji wa mazingira mazuri ya kuibua fursa za kiuchumi
Vyombo vya habari	<ul style="list-style-type: none"> ☞ Ushirikiano ☞ Habari sahihi; ☞ Uwazi;

CHAPTER TWO

2.0 VIWANGO VYA HUDUMA

2.1 IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kutoa miongozo ya utendaji wa kazi na kuisambaza kwa watumishi.	Tutatoa miongozo ya utendaji wa kazi ndani ya siku moja ya kazi.
2	Kupandisha vyeo vya watumishi na kuthibitisha kazini watumishi	Tutafanya mchakato wa kupandisha vyeo watumishi ndani ya siku 30 za kazi
3	Kushughulikia Uhamisho wa watumishi kwenda nje na kuingia Halmashauri ya Mji Kibaha.	Tutapitisha maombi ya uhamisho ndani ya siku moja tangu kuwasilishwa kwa maombi
4	Kusikiliza matatizo ya watumishi na shida zao.	Tutasikiliza kila siku za kazi.
5	Kuhakikisha watumishi wote wanajaza Fomu za OPRAS.	Siku 7 za kazi kwa kila mwezi
6	Kuidhinisha likizo na madai ya malipo ya likizo ya watumishi.	Siku 14 za kazi.
7	Kuandaa mafao ya wastaafu ili kurudi kwao	Tutandaa ndani ya siku 2 ya kazi.
8	Kuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi na madiwani.	Mpango utaandaliwa ndani ya siku 14 za kazi.
9	Kushughulikia uteuzi wa watumishi wanaotakiwa kwenda masomoni.	Siku 14 za kazi.
10	Kufuatilia kadi za bima ya afya kwa ajili ya kuwapatia watumishi.	Tutafuatilia ndani ya siku saba za kazi.
11	Kushughulikia na kuomba kibali cha ajira mpya na kupandisha cheo.	Ajira mpya zitashughulikiwa ndani ya siku 30 za kazi.
12	Kutafuta na kupeleka jalada kwa afisa anayetakiwa kulishughulikia.	Dakika 35 tangu ombi kupokelewa masjala kuu ya Halmashauri.
13	Kushughulikia barua za maombi mbalimbali yanayoletwa idarani.	Maombi yatashughulikiwa ndani ya siku 3 tokea maombi kuwasilishwa.
14	Kuandaa bajeti ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri	Bajeti itaandaliwa ndani ya siku 30 za kazi.
15	Kuandaa bajeti ya matumizi ya mafunzo na matumizi mengineyo kwa idara ya utumishi na utawala.	Bajeti itaandaliwa ndani ya siku 30 za kazi
16	Kusimamia matumizi mazuri ya vyombo vya usafiri.	Siku 7 za wiki
17	Kusimamia matengenezo ya magari ya halmashauri ya mji	Siku 7 za wiki
18	Kusimamia utendaji kazi wa watumishi wote	Siku 7 za wiki

19	Kufanya maandalizi ya vikao vya kisheria vya Halmashauri.	Siku 7 za wiki
----	---	----------------

SEKTA YA MALALAMIKO

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kupokea na kusikiliza kero na malalamiko ya wananchi na watumishi na kuyaandikisha	Siku 1 ya Wiki
2	Kuingiza na kuhifadhi taarifa za malalamiko kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano na kutumia taarifa za mawasiliano kuonesha maeneo ya kufanyia kazi.	Siku 1 za kazi kero ndogo ndogo na siku 30 kwa kero kubwa.
3	Kufanya uchambuzi wa awali wa malalamiko	Siku 2 ya kazi.
4	Kuwasilisha malalamiko kwenye idara au kitengo kwajili ya kupatiwa ufumbuzi	Dakika 1 za kazi.
5	Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kazi za idara za robo, nusu na mwaka mzima.	Siku 7 ya kazi.
6	Kushughulika malalamiko ya wananchi kuhusu kutokuwepo na huduma za jamii kwa kuwaelimisha	Siku 5 ya kazi katika kata 11.
7	Kutoa ushauri kwa wateja	Kila siku ya kazi.
8	Kufungua masanduku ya maoni na kuyachambua na kuyatafutia ufumbuzi.	Siku 3 za kazi.
9	Kuwasilisha taarifa ya kero na malalamiko kwa mkurugenzi mtendaji na taasisi ya kuzuia rushwa	Siku 5 za kazi.
10	Kufuatilia Malalamiko yanayoshughulikiwa na idara au kitengo	

2.1.2 OFISI ZA KATA

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Mtendaji wa kata kusikiliza kero na malalamiko na kuyatatua.	Siku 1 ya kazi.
2	Kusimamia utekelezaji wa miradi ya mendeleo katika kata	Kila siku za kazi.
3	Kusimamia na kukagua usafi wa mazingira katika kata.	Siku 1 ya kazi katika kila kata.
4	Kuhamasisha ulinzi na usalama kwa kufanya mikutano.	Siku 1 ya kazi kila kunapofanyika Kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata.
5	Kuhakikisha watendaji wa mitaa wanasimamia ulinzi na usalama katika mitaa yao.	Siku 1 ya kazi kila baada ya miezi miwili.
6	Kusimamia chaguzi za serikali za mitaa na serikali kuu. (Aro-kata)	Kipindi chote cha uchaguzi.
7	Kusimamia uandikishwaji wa wapiga kura. (Aro-kata)	Kipindi chote cha uandikishwaji wa wapiga kura.
8	Kufuatilia utoaji wa huduma za jamii katika kata.	Siku 1 ya kazi kwa kila sekta.

2.2. KITENGO CHA SHERIA

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kumshauri Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu mambo ya kisheria.	Kila siku za kazi.
2	Kushughulikia kesi mahakamani za kushtaki au kushtakiwa Halmashauri..	Kila siku za kazi kesi inapotajwa mahakamani.
3	Kusaini fomu za dhamana.	Dakika 3.
4	Kutunga rasimu za sheria ndogo ndogo za Mji Kibaha.	Siku 60 za kazi.
6	Kuatayarisha mikataba ya Halmashauri.	Siku 7 kwa kila mkataba.
7	Kufuatilia utekelezaji wa sheria ndogo ndogo na kuandika taarifa.	Siku 2 za kazi.
8	Kuandaa bajeti ya mabaraza ya kata.	Siku 7 za kazi.
9	Kuwafundisha wajumbe wa mabaraza ya kata juu ya kanuni na taratibu uendeshaji wa mabaraza.	Siku 2 za kazi mara baada ya uchaguzi.
10	Kumshauri Mkurugenzi na watendaji wake mambo ya kisheria katika vikao vya uongozi.	Kila siku ya vikao.
11	Kutayarisha bajeti ya kitengo.	Siku 7 za kazi.
12	Operesheni ya kukagua usafi kwa kushirikiana na maafisa wa afya.	Siku 30 za kazi.

2.3. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kukagua na kutoa taarifa ya mapato ya Halmahauri ili kuhakikisha taratibu za fedha zimefuatwa.	Siku 1 ya kazi kila robo mwaka.
2	Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo ya Halmashauri kama taratibu zimefuatwa (Value for Money).	Siku 1 ya kazi kwa kila mradi.
3	Kukagua mikataba ya wakandarasi kama taratibu za fedha na nyaraka zilizoambatanishwa zinakidhi kanuni na taratibu za fedha za serikali.	Siku 2 za kazi.
4	Kukagua risiti za urejeshaji masurufu.	Siku 1 ya kazi.
5	Ukaguzi wa robo mwaka na kutoa taarifa yake	Siku 9 au 10 baada ya robo ya mwaka kukamilika
6	Ushauri kwa wahasibu	Mara tu inapoonekana umuhimu wakufanya hivyo
7	Kukagu miradi ya maendeleo programu 1 hadi 2 kwa robo mwaka na taarifa zake kutolewa	Siku 9 hadi 10 baada ya zoezi la ukaguzi kumalizika

8	Kuandaa mpango kazi wa ukaguzi wa ndani na kuwasilisha Ofisi ya Taifa ya ukaguzi ngazi ya mkoa.	Siku 10 hadi 12 baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha
9	Kufanya kazi zingine maalum kabla zitakavyojitokeza	Wakati zitakavyojitokeza

2.4. KITENGO CHA MANUNUZI

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kuomba kibali cha kununua bidhaa kutoka kwa maafisa wanaohusika kwa kujaza fomu.	Dakika 5 za kazi.
2	Kujaza fomu za zinazoonyesha bidhaa zinazohitajiwa na kusainiwa na mkuu wa kitengo.	Dakika 5 za kazi.
3	Kutangaza zabuni katika magazeti.	Siku 2 za kazi.
4	Kuchagua wazabuni watakaotoa huduma katika halmashauri.	Siku 60 za kazi.
5	Kumkabidh mzabuni nyaraka zinazoonyesha aina za bidhaa zinazohitajika.	Siku 1 ya kazi.
6	Kupokea bidhaa zilizounuliwa na mzabuni na kuweka stoo.	Siku 1 ya kazi.
7	Kuwaatarifu wazabuni waonyeshe gharama za kutoa huduma.	Siku 1 ya kazi.
8	Kufungua na kutangaza bei zilizotolewa na wazabuni.	Masaa 2 ya kazi.
9	Kuteua wajumbe watakaotoa tathmini maombi ya dhabuni na kumpata mshindi.	Siku 40 za kazi.
10	Kumpatia barua na mkataba mzabuni aliyeshinda.	Siku 14 za kazi.

2.5. KITENGO CHA UCHAGUZI

1	Kutembelea vituo 114 vya Uchaguzi kwenye kata 11 na mitaa 53	Kila robo siku 10
2	Kukagua Vituo 114 vya uchaguzi	Siku 5 za kazi
3	Kuboresha Daftari la wapiga kura kwa kata 11 na vituo 114	Siku 14
4	Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	Siku 14
5	Kusimamia Uchaguzi mkuu	Siku 30
6	Kusimamia Chaguzi Ndogo za mitaa na Uchaguzi Mkuu	Siku 30
7	Kuandaa ripoti za chaguzi za Serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu	Siku 7

2.6. KITENGO CHA NYUKI

1	Kuhamasisha wananchi wafuge nyuki ili wainue vipato vyao.	Siku 7 za kazi.
2	Kutoa elimu juu ya ufugaji nyuki	Saa 1
3	Kutoa taarifa zinazohusu ufugaji nyuki kama vile idadi ya mizinga ya nyuki, wafugaji, uzalishaji wa asali na nta.	Saa 1
4	Kuhamasisha ufugaji bora wa nyuki	Saa 1 – 3
5	Ukusanyaji wa maduhuli	Saa 1
6	Kukusanya takwimu kuhusu nyuki, utalii	Saa 1 – 3
7	Kuandaa sheria ndogo za ufugaji nyuki	14 za kazi
8	Kusimamia viwango vya ubora wa mazao ya nyuki	14 za kazi
9	Kusimamia uanzishaji wa hifadhi za nyuki na manzuki	30 za mwaka

10	Kukusanya Takwimu za Rasilimali na Ufugaji Nyuki na kutoa taarifa TAMISEMI	Kila robo ya mwaka
11	Kufundisha na kuelimisha wananchi juu ya ufugaji nyuki	7 days

2.7. KITENGO CHA TEKNOLOGIA, HABARI NA MAWASILIANO

2. 7.1 HABARI

1	Kuratibu Shughuli za Machapisho ya Halmashauri	Kila 1 ya kazi
2	Kutayarisha News letter(taarifa za kila idara)	Mara mbili kwa mwaka
3	Kuelezea umma namna miradi inavyotekelezwa	Kila siku ya kazi
4	Kuoa taarifa kwa umma juu ya uwepo wa Baraza la wazi la madiwani	Kila robo
5	Kupiga picha ya matukio muhimu ya kiserikali na halmashauri	Kila siku za kazi
6	Kuweka kumbukumbu ya matukio ya kitaifa na halmashauri yanapotokea	Kila siku za kazi
7	Kutoa taarifa mabalimbali kwa wadau wa halmashauri	Kila siku za kazi
8	Kuhakikisha taarifa kwenye mtandao wa halmashauri unakuwa salama	Kila siku za kazi
9	Kushikiki na kutoa matangazo juu shughuli za Halmashauri	Kila siku za kazi
10	Kushiriki katika vikao vya kazi vya maafisa habari na kutoa taarifa za utekelezaji wa kazi	Mara tatu kwa mwaka

2.7.2-TEKNOLOGIA NA MAWASILIANO

1	Kufanya matengenezo ya awali ya computer zote za halmashauri	Kila robo
2	Kutoa msaada wa kiufundi kwa watumishi wote wanaotumia computer na mifumo ya ya computer	Kila siku ya kazi
3	Kuweka kumbukumbu ya vifaa vya computer vyote	Kila robo
4	Kuhakikisha kikoa,barua pepe na tovuti vinafanya kazi mda wote	Kila siku
5	Kumshauri Mkurugenzi wa Halmashauri juu ya vifaa vipya, na mifumo laini mipya inayoweza kutumika	Kila robo
6	Kuelimisha wafanyakazi juu ya matumizi sahihi ya computer	Mara 2 kwa mwaka
7	Kuhakikisha Computer Zinafanya kazi pamoja na kuweka programme sahihi kwenye computer	Kila siku

2.8. IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

2.8.1 SEHEMU YA KUFUNGA HESABU.

NA	HUDUMA ZINAZOHUSIKA	MUDA
1	Uandaaji wa taarifa mbalimbali za fedha kila mwezi na robo mwaka.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 3 hadi 5 mara baada ya kufunga hesabu za mwezi..
2	Uandaaji wa Usuluhisho wa kibenki.	<ul style="list-style-type: none"> Muda wa siku 3 baada ya kupokea taarifa za kibenki.
3	Kuandaa “General Ledger” kila mwezi kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 2 baada ya mwezi kuisha.
4	Kuandaa “Trial Balance” kila mwezi kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 2 baada ya mwezi kuisha.
5	Kuandaa “Income Statements” na “Balance Sheet” kila mwezi na kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 3.
6	Kuandaa “Quarterly Consolidated”, “Trial “Balance”, “Income Statements”, na “Balance Sheet”.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 5.
7	Kuandika “Fixed Assets” “Register”.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 5 kwa kila mwamala.
8	Kuandaa “Recurrent Budget’ na kuiwasilisha sehemu husika.	<ul style="list-style-type: none"> Muda wa miezi 4(Januari - April).
9	Kuandaa/Kufunga hesabu za mwisho wa mwaka. Kwa Idara zote za Halmashauri kuanzia mwezi Julai hadi Septemba. Pamoja na kuiwasilisha kwa wadau husika.	<ul style="list-style-type: none"> Miezi 3.
10	Kuandaa taarifa zarobo mwaka na kuzituma kwa RAS, TAMISEMI na kuwasilisha katika vikao vya kisheria.	<ul style="list-style-type: none"> Siku tano (5).
11	Kuandaa “Budget Statements” kila mwezi na kila mfuko..	<ul style="list-style-type: none"> Siku tano (5).
12	Kujaza Rejista ya Masurufu kwa wanaochukua na kurejesha masurufu kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 kwa kila muamala.
13	Kuandaa “Imprest/ Advance” “Position Monthly” kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Siku 5.
14	Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya LAAC.	<ul style="list-style-type: none"> Kila baada ya miezi 3.

2.8.2 SEHEMU YA MAPATO.

NA	HUDUMA ZINAZOHUSIKA	MUDA
1	Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya halmashauri na kufanya ufuatiliaji.	<ul style="list-style-type: none"> Siku 2 kila wiki.

2	Kuitisha na kukagua vitabu vya wakusanya Mapato kila baada ya miezi mitatu (3) au wakati wowote itakapo lazimu.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 15 kwa kila mkusanya mapato. Mwenye vitabu visivyozidi/Kupungua vitabu 5.
3	Kupokea fedha kutoka kwa watendaji/ wakusanya mapato.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 5 kwa kila mkusanya mapato. Kwa mtu aliye na vitabu visivyozidi 3.
4	Kuandaa Muhtasari wa Mapato kwa kila mfuko. Mwishoni mwa mwezi na kutoa taarifa ya Mapato.	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku mbili (2).baada ya mwezi kuisha
5	Kukatia stakabadhi fedha kutoka hazina na sehemu nyinginezo.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 10 kwa “Bank Statement” zisizozidi 10.
6	Kunukuu, rejista za madeni, na wazabuni mbalimbali wanaokusanya mapato.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 5 kwa rejista mbili (2).
7	Kupeleka fedha benki zilizopokelewa kila siku. Kuanzia saa 8:00 mchana.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 10 mpaka 30 kuna tegemea foleni iliyopo benki.
8	Kunukuu Mapato katika vitabu vya fedha “(Cash book)” kila siku kuanzia saa 9:00 Alasiri.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 10 na kuendelea kunategemea Miamala iliyopo.
9	Kunukuu “Miscellaneous deposits register” kwa mchanganuo.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 10 za jioni kuanzia saa 10:00 jioni. Kila siku.
10	Kuandika Stakabadhi kwa hundi zote za 1% kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> Siku 1 katika wiki.
11	Kutoa vitabu vya kukusanyia mapato kwa wakusanya Mapato.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 kwa kila kitabu pamoja na kukisajili .
12	Kupokea vitabu vilivyokwisha tumika mara baada ya kutumika na kuhakikiwa.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 kwa kila kitabu.

2.8.3 SEHEMU YA MATUMIZI.

NA	HUDUMA ZINAZOTOLEWA	MUDA
1	Kusimamia Mtiririko mzima wa malipo kwa kuzingatia uharaka, usahihi kwa kufuata taratibu, Kanuni na sheria za fedha.	<ul style="list-style-type: none"> Kila Siku kuanzia saa 1.30 Asubuhi mpaka saa 9.30 alasiri.
2	Pre audit itafanyika kwa kila hati ya malipo iliyokamili. Ikiwa ni kuwepo kwa sahihi zote. Kuanzia muandaaji wa malipo, mkuu wa Idara na Mweka hazina. Pia kuwepo kwa viambatanishi vyote vyenye ruksa ya Mkurugenzi Mfano: - barua, LPO, Requisition, Quotations, Delivery note, Invoice, fomu ya maombi, No. 1, 2, 3, Muhtasari wa kikao, na	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 mpaka 5 kwa kila hati moja ya malipo.

	mikataba kama italizimika.	
3	“Vote - book” kila mhasibu wa Idara /Mfuko atajaza “vote book”. Kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu za fedha. Malipo yatakayoingizwa katika “vote book” ni yale tu yaliyo ndani ya bajeti iliyokisiwa.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 mpaka 5 kwa kila ombi 1 lililofika mezani kwa mhasibu wa mfuko.
4	Uandishi wa hati za malipo utafanyika kwa maombi yote ambayo hayajazidi bajeti, na yamekamiliwa kwa kibali cha Afisa Mhasibu (Mkurugenzi Mtendaji). Na kwa madai yote yaliyozingatia sheria na kanuni za fedha.	<ul style="list-style-type: none"> Dakika 3 kwa kila hati moja ya malipo baada ya kuhakiki viambatanishi.
5	“Check Room” - hundi zote zitakazo weza kuandikwa nizile tu ambazo madai yake yamefuata sheria na taratibu za fedha.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 2 kwa kila hati moja ya malipo baada ya kuhakikiwa.
6	Utoaji wa hundi kwa wateja - hundi zote zinazotolewa zitasajiliwa katika rejista na mteja atasaini ndipo ataweza kuchukua.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 3 kwa kila hundi baada ya kuisajili.
7	Malipo ya fedha taslimu kwa watumishi wanaozidi mtu mmoja katika madai yatalipwa na “Cashier” wa matumizi.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 2 mara baada ya fedha hizo kufika kutoka benki.
8	Kunukuu “Check list” kwa malipo yote ambayo yameandikiwa hundi kwa kila mfuko	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 5. Kwa “check list” moja ya mfuko.
9	Kupeleka “Check list” na malipo yake kwa Mweka hazina /Mkurugenzi Mtendaji kwa sahihi.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 1 mara baada ya mzunguko mmoja kukamilika.
10	Mishahara kufuata Payroll Iringa na kuzileta Njombe.	<ul style="list-style-type: none"> Muda wa siku 1.
11	Kuchambua mishahara kufanya usuluhisho wa mishahara na kupeleka kwa wakuu wa Idara kwa uhakiki wa watumishi kabla ya kufanya malipo.	<ul style="list-style-type: none"> Muda wa siku 1.mara baada ya TT na Payroll kufika
12	Kuandika hati za malipo za mishahara za kulipia pamoja na hati za malipo za kuhamisha fedha toka A/C No. 1, na 3 kwenda mifuko ya kulipia pamoja na kusainisha. Kwa wakuu wa Idara husika.	<ul style="list-style-type: none"> Muda wa siku 1.mara baada ya Payroll kuhakikiwa na wakuu wa idara husika.
13	Kukagua/Kufanya ukaguzi wa awali kwa mishahara yote.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 60.mara baada ya Payroll kusainiwa na wakuu wa idara na kuidhinishwa na Ofisa Mhasibu na Mtunza Hazina
14	Kuandika hundi zote za mishahara na kuhamisha fedha za mishahara.	<ul style="list-style-type: none"> Muda dakika 45.mara baada ya ukaguzi wa awali kufanyika.
15	Kuchambua Makato yote ya kisheria na kuandika hati	<ul style="list-style-type: none"> Muda siku 1.mara baada ya

	za malipo kwa makato yote pamoja na kusainisha wakuu wa Idara husika. Na Mweka hazina kwa kuidhinisha hati hizo, Ikiwa ni pamoja na kuomba kibali cha kuhamisha makato hayo kwenda katika mifuko ya kulipia.	mihahara kulipwa/kukamilika
16	Kufanya ukaguzi wa awali kwa malipo yote yanayohusu makato ya mishahara.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda dakika 60. Mara baada ya kuidhinishwa na mamlaka husika.
17	Kuandika hundi zote za makato pamoja na “check list” za makato ya mishahara.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda dakika 45. Mara baada ya ukaguzi wa awali kukamilika
18	Kufanya marekebisho ya mishahara ya watumishi.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda dakika 5 kwa faili moja.
19	Kuandika/Kunukuu vitabu vya fedha - matumizi “(cash book)” kwa kila mfuko hundi zilizoandikwa.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda dakika 1 kwa kila muamala.
20	Kufanya “Balancing” kwa kila “Cash book”.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda dakika 10 kwa “(cash book)” yenye “Transactions” zisizozidi kumi.
21	Kujibu hoja za Mkaguzi wa ndani na wa nje. Mara baada ya hoja kuibuliwa.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda siku 21 mara baada ya hoja za ukaguzi kuwasili.
22	Kusaini Mihtasari ya malipo na hundi toka vijijini baada ya ukaguzi/ uhakiki.	<ul style="list-style-type: none"> • Dakika 5 kwa kila Muhtasari uliokaguliwa.
23	Kukagua miradi kwa ajili ya malipo ya wazabuni mbalimbali.	<ul style="list-style-type: none"> • Muda siku 2.
24	Kusaini hati za malipo hundi na “cheque list” baada ya uhakiki.	<ul style="list-style-type: none"> • Dakika 1 kwa kila hati ya malipo • Dakika 1 kwa kila hundi. • Dakika 5 kwa kila “check list”.
25	Kufanya “Soft Copy Posting” kwa kila mfuko.	<ul style="list-style-type: none"> • Dakika 30 kwa kila “Transactions” 60.

2.8.4 SEKTAYA BIASHARA

NO	HUDUMA ZINAZOTOLEWA	MUDA
1	Kutoa leseni kwa wafanya biashara wanao hudumiwa na Halmashauri ya Wilaya.	Muda wa siku mbali
2	Ukaguzi wa kata mbili	Muda wa juma moja
3	Mafunzo kwa wajasiriamali 30 watakao kuwa wamearifiwa kutoka kwenye kata zitakazo kuwa zimechaguliwa	Muda wa siku tatu
4	Kuandika mpango wa biashara(business plan) ili kuwasaidia wafanyabiashara kujua mbinu za kibiashara na kupata mikopo katika vyombo vya fedha	Muda wa juma moja

5	Kutoa elimu ya biashara kwa wafanyabiashara na jinsi ya kupata faida katika biashara zao	Muda wa juma moja
---	--	-------------------

2.9. IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kuandaa bajeti ya Halmashuari ya Mji Kibaha	Siku 90 za kazi.
2	Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Mji Kibaha.	Siku 7 za kazi.
3	Kukusanya takwimu kuhusu hali ya kiuchumi ya Halmashauri ya Mji Kibaha.	Siku 90 za kazi.
4	Kukusanya takwimu za mfumo wa ufuatiliaji na tahmini za serikali za mitaa.	Siku 30 za kazi.
5	Kutoa ushauri kwa jamii kuhusu tafiti na takwimu.	Siku 7 za kazi.
6	Kuchambua sera za kitaifa na kuzifikisha ngazi za chini.	Siku 7 za kazi.
7	Kuratibu mafunzo ya uimarishaji mipango na ushirikishwaji jamii katika kupanga mipango ya maendeleo na utekelezaji wake.	Siku 30 za kazi.
8	Kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kila robo mwaka.	Siku 7 za kazi.
9	Kuratibu upimaji wa Halmashauri dhidi ya masharti ya kupata fedha za maendeleo.	Siku 30 za kazi.
10	Uandaaji wa Taarifa mbalimbali kwa kila robo na mwaka nzima	Siku 24 za kazi
11	Kusimamia zoezi la ukusanyaji wa takwimu mbalimbali zikiwemo zile za wasifu wa kiuchumi na kijamii wa Halmashauri na takwimu za fursa za uwekezaji na kuziunganisha	Siku 60 za kazi
12	Kufanya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya matumizi ya Halmahauri	Siku 60 za kazi
14	Maandalizi ya Mpango kazi (Action plan) kwa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida	Siku 60 za kazi
15	Kuandaa Maandiko ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya kutafuta fedha kwa wadau mbalimbali wa maendeleo	Siku 90 za kazi
16	Ukaguzi wa shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo	Siku 120 za kazi
17	Kuandaa mipango mkakati za Idara mbalimbali za Halmashauri	Siku 20 za kazi

2.10. IDARA YA ELIMU YA MSINGI

NA	HUDUMA	MATARAJIO
1	Kupata takwimu ya watoto wenye miaka mitano.	Siku 14 za kazi.
2	Kufuatilia uandikishwaji wa watoto wanaostahili kupata elimu ya awali.	Siku 14 za kazi.
3	Kuhakikisha waalimu wanatosholeza katika shule za elimu ya awali.	Siku 14 za kazi.
4	Kukagua kama waalimu wa shule za elimu ya awali wanaingia darasani.	Siku 14 za kazi na mara mbili kwa mwaka.
5	Kuhakikisha elimu bora inatolewa shule za msingi kwa kuhakikisha waalimu wenye taaluma wanatosheleza, zana za kufundishia zipo, na kuna vitabu vya ziada na kiada.	Siku 30 za kazi kila baada ya miezi sita.
6	Kupata takwimu za watoto wenye miaka 5 hadi 7.	Siku 7 za kazi.
7	Kuelimisha jamii kupitia kamati za shule za msingi ili kujua umuhimu wa elimu kwa watoto wao.	Siku 1 ya kazi kila kamati za shule zinapokutana.
8	Kupeleka fedha mashuleni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.	Siku 1 ya kazi kila baada ya miezi mitatu.
